MEDIA BRIEFS FOR MoM APRIL 30, 2019

HABARILEO

- **JPM aagiza kiwanda cha Kiwira kifufuliwe**

Rais John Magufuli amemwagiza Waziri wa Madini Doto Biteko kukamilisha malipo ya madeni pamoja na kuhakikisha hisa za asilimia 70 za Kampuni ya Tanpower Resources kuja serikalini ili Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira uanze kazi mara moja. Alitoa maagizo hayo jana alipokuwa Kiwira mkoani Mbeya wakati akiwahutubia wananchi wa eneo hilo waliojitokeza kwa wingi barabarani. Rais Magufuli yupo mkoani humo kwa ziara ya kikazi. (Uk.4).

- **Majaliwa: Sadc hakikisheni usalama uchimbaji wa urani**

Waziri Mkuu, Kassim Maaliwa amewataka washiriki wa Mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) unaoadili mambo ya nyuklia, kuhakikisha usalama wa watu, mazingira na mfumo wa kijiolojia unazingatiwa katika eneo la SADC kwa mujibu wa sheria. Alitoa mwito huo jana jijini Arusha wakati akifungua mkutano wa wataalam wa mionzi kutoka nchi za kusini mwa Afrika. (Uk.4).

- **DC Chunya amkosha JPM kwa miradi**

Mikakati kabambe ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuwainua wachimbaji wadogo vimetajwa kuwa miongoni mwa mambo yaliyomfanya Rais John Magufuli kumwagia sifa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mary Prisca Mahundi kwa kuchapa kazi nzuri. Tangu alipoteuliwa kushika nafasi wilaya ya Chunya, Mahundi amekuwa anaweka mikakati mbalimbali kuboresha usimamizi wa miradi ya maendeleo na kuchukua hatua za kuwakomboa wachimbaji wadogo kuzuia utoaji kodi zisizo kisheria. (Uk.19).

UHURU

- **Madudu mengine yashtukiwa Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira**
- **Ni kuhusiana na madai hewa ya mabilioni... JPM ampa nafasi Waziri Biteko kufafanua**

Hatimaye madudu mengine ya Mgodi wa Makaa ya Mawe, yameshtukiwa yakiwemo madai hewa ya mabilioni ya fedha ambayo yaliwasilishwa serikalini. Rais Dkt. John Magufuli ambaye yuko kwenye ziara mkoani Mbeya, alimtaka Waziri wa Madini Doto Biteko kutoa sababu za mgodi huo kutofanya kazi.....Akizungumza mbele ya wananchi hao, Waziri Biteko alisema mgodi huo ulikuwa ukifanya kazi tangu serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani mwaka 2015. Biteko alisema kusimama kwa mgodi huo kulitokana na kampuni iliyokuwepo ya TanPower Resources kuamua kuondoka kisha kurudisha mgodi serikalini. (Uk.1& 2).

- **Wachina waja kuwekeza sekta ya madini**

Naibu Waziri wa Madini Doto Biteko amesema serikali ya awamu ya tano imeweka mazingira mazuri ya kuwekeza nchini, kupitia sekta ya madini na kuwataka wageni kutosita kutembelea maeneo mbalimbali ili kujionea fursa zilizopo na kuwekeza. Nyongo aliyasema hayo juzi wakati akipokea ujumbe ulioongozwa na Naibu Waziri wa Maliasili kwa ajili ya kujadili maeneo ya kushirikiana katika sekta ya madini baina ya Tanzania na China. (Uk.8)

FAHARI YETU

- **Kampuni za uchenjuaji wa madini zatakiwa kufuata sheria**

Kampuni za uchenjuaji wa madini ya Dhahabu wilayani kahama mkoani Shinyanga, zimetakiwa kufuata sheria za madini na kulipa maduhuli ya serikali kwa wakati ili kuweza kuondoa migongano ya malalamiko yanayoweza kujitokeza baina ya pande zote mbili. Kwasasa nchi inategema kwa kiasi kikubwa kodi kwa ajili ya kuendesha shughuli za maendeleo kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo yakiwemo makampuni hayo ambayo yanajishughulisha na uchenjuaji wa madini. Ofisa Uhusiano wa kampuni inayojishughulisha na uchenjuaji wa dhahabu Busami wilayani Kahama Shida Soko alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na vyombo vya abarri ofisini kwake ambapo alisema kuwa, kampuni zikilipa kodi kwa wakati inaweza ikawa moja ya sababu ya kufanya hata

wachimbaji wadogo kuwa na amani wanapokwenda kufanya shughuli za uchenjuaji. (Uk.5).

JAMVI LA HABARI

- **Kampuni yapewa miezi sita kufunga mgodi wa dhahabu**

Mkaguzi Mkuu wa migodi nchini Abdulrahman Mwanga ametoa miezi sita kwa kampuni ya dhahabu ya Shanta iliyopo Mbagala wilayani Songwe mkoa wa Songwe, kuwasilisha andiko la kufunga mgodi wake wa New Luika Gold Mining ambao unatarajiwa kumaliza muda wake ifikapo mwaka 2023 kwa mujibu wa mkataba. Mwanga ameyasema hayo jana wakati wa ukaguzi wa migodi yote ya kampuni ya Shanta akidai licha ya mambo mazuri yanayofanywa na kampuni hiyo, bado kuna dosari katika mkakati wa kurejesha mazingira katika hali yake ya kawaida baada ya kukamilisha uchimbaji wa dhahabu. (Uk.5)

- **Nyongo kupokea ujumbe wa watu kumi kutoka China**

Naibu Waziri wa Madini Stanslaus Nyongo amepokea ujumbe ulioongozwa na Naibu Waziri wa Maliasili wa Jamhuri ya Watu wa China waliofika kwa ajili ya kujadiliana maeneo ya ushirikiano katika sekta ya madini baina ya Tanzania na China. Akizungumza wakati akifungua kikao cha majadiliano jijini Dar es Salaam jana, Nyongo aliwahakikishia wageni hao kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imeweka mazingira mazuri ya kuwekeza nchini kupitia sekta ya Madini na kuwataka kutosita kutembelea maeneo mbalimbali ili kujionea fursa zilizopo na kuwekeza Tanzania. (Uk.8).

MAJIRA

- **Nyongo apokea ujumbe wa watu 10 kutoka China (Uk.7)**

Habari katika picha- Naibu Waziri wa Madini Stanslaus Nyongo akiwa na Naibu Wazii wa Maliasili wa China, Dkt. Zhong Ziran pamoja na wajumbe waliombatana nao kutoka pande hizo mbili mara baada ya kumaliza kikao kilichofanyika baada ya ugeni kutoka China kuwasili nchini juzi. (Uk.7).

- **Mgodi waahaidi kuleta madaktari bingwa Mara**

Kutokana na changamoto ya upungufu mkubwa wa madaktari bingwa unaozikabili hospitali za wilaya za Mkoa wa Mara, Kampuni ya Acacia kupitia Mgodi wa North Mara uliopo Nyamongo wilayani Tarime mkoani Mara, umeahidi kuendelea kuhifadhi madaktari hao kutoka mikoa mbalimbali nchini. Lengo ikiwa ni kuja wilayani Tarime na maeneo mbalimbali mkoani Mara ili kutoa huduma za matibabu kwa wananchi kutokana na wananchi wengi kushindwa kumudu gharama za matibabu. (Uk.7)

- **Siri ya Magufuli kukunwa na DC wa Chunya yabainika**

Mikakati kabambe ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuwainua wachimbaji wadogo vimetajwa kuwa miongoni mwa mambo yaliyomfanya Rais John Magufuli kumwagia sifa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mary Prisca Mahundi kwa kuchapa kazi nzuri… Akiwa ziarani wilayani humo juzi, Rais Magufuli alisema 'Nakupongeza sana Mkuu wa wilaya (Mahundi) unafanya kazi kubwa sana".....Akizungumzia sekta ya madini, Rais Magufuli alitoa msisitizo mkubwa wa viongozi wa wilaya , Mkoa na Waziri wa Madini, Doto Biteko kuwasaidia wachimbaji wadogo na alipongeza hatua zinazoendelea kuchukuliwa na uongozi wa wilaya hiyo katika kuwwatafutia maeneo mazuri ya uchimbaji. Akizungumza mbele ya Rais Magufuli, Mkuu huyo wa wilaya hiyo alisema kutokana na wilaya hiyo kuwa namba moja mkoani mbeya katika uzalishaji wa madini, hatua mbalimbali zinachukuliwa ili kuhakikisha Taifa linanufaika na rasilimali madini. (Uk.11).

MWANANCHI

- **Gari lililokamatwa na dhahabu lakwamisha usikilizwaji kesi**

Gari walilokutwa nalo washtakiwa wa kesi ya jinai namba 1/2019 ya kusafirisha kilo 319 za dhahabu zenye thamani ya Sh 27.18 bilioni na fedha taslimu sh 305 milioni imesababisha shauri hilo lishindwe kuendelea baada ya pande mbili kuvutana kwa hoja mahakamani. Hatua hiyo ilifikiwa jana baada ya shahidi namba moja, Maximiliani Katabazi, kuanza kutoa ushahidi mbele ya Hakimu Mkazi

Mfawidhi wa Mahakama ya Mkowa wa Mwanza Rhoda Mgimilanga. (Uk.8)

DAILYNEWS

- **Hasten Kiwira shares transfer**
- **President directs Minerals Minister Biteko**

President John Magufuli has directed Minerals Minister Doto Biteko to hasten transfer of 70 percent stake in Kiwira Coal and Power Limited (KCPL) from Tan Power Resources Limited (TPR) to the government. The transfer of the shares from investor to the State will pave the way for other potential investors who have shown interest in the project to commence excavation of coal to generate electricity. (Uk.1 &3).

- **Chinese Geologists, Vice Minister in Dar to improve local mining industry**

Some Chinese Geologists along with their Vice Minister for Natural Resources of China are in Dar es Salaam for a five - discussion with Tanzania's government on how to improve the latter's mining sector and enable the government increase its income through the industry. The Deputy Minister for Minerals, Mr. Stanslaus Nyongo said the Chinese are in talks with the government to cooperate in improving Tanzania's geological survey and in turn enable the country open much in minerals. (Pg.8).